TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA

Food and Agriculture Organization of the United Nations

TARI

Ministry of Agriculture, Food and Rural Affairs Republic of Korea

# KITALU MKEKA KILICHOBORESHWA





## kitalu mkeka ni nini?

Kitalu mkeka ni uoteshaji wa miche ya mpunga katika udongo iliyochanganywa na samadi na kusambazwa kina kifupi juu ya ardhi iliyosawazishwa na isiyoruhusu mizizi kupenya

Miche hii inakuwa tayari kupandwa ndani ya siku 8 - 14 baada ya kuota





## Faida za kitalu mkeka

- Kinatumia ardhi ndogo, meta za mraba 40 zinatosha kwa shamba la ekari 1
- Kinaweza kuoteshwa karibu na nyumba kuliko vitalu vya jadi vya shambani
- Inahitaji mbegu chache na kiasi kidogo cha pembejeo
  kama vile mbolea na maji, hivyo kupunguza gharama za kitalu hadi 50%
- Kutenganisha miche kabla ya kupandikiza ni rahisi, hivyo kupunguza uharibifu wa mizizi
- Hurahisisha usafirishaji
- Na, muhimu zaidi, hutoa miche yenye afya na inayokua haraka, ambayo hutoa mavuno mengi



## Eneo la Kitalu mkeka

- Meta za mraba 40 kwa ajili ya kupanda shamba la ekari 1 moja)
- Kitalu kilichonyanyuka

⇒ Urefu = 5 cm.

⇒ Upana = 1 m.




## Vifaa

1. Karatasi ya plastiki (nailoni) au kipande cha gunia (kisalfeti) au majani ya migomba
2. Mchanganyiko wa udongo na samadi (1:1) au udongo peke yake kama una rutuba ya kutosha
3. Fremu yenye vyumba vyenye ukubwa wa eneo la meta za mraba 0.25 (upana m 0.5 na urefu m 0.5) na kina cha sm 5
4. Keni ya kumwagilia (watering cane)





## Mahitaji

1. Kiuatilifu kwa ajili ya kuua fangasi na bakteria
2. Mbegu iliyoatamishwa au ambayo haijaatamishwa
3. Mbolea ya DAP au NPK
4. Samadi
5. Maji



Kuchanganya udongo, samadi na mbolea



Jaza mchangayiko wa udongo na mbolea kwenye fremu



Mahitaji ya Mbegu

- Kilo 2 – 3 kwa ajili ya shamba la ekari 1 kwa kupandikiza kwa nafasi pana ya sm 25 x 25
- Gramu 25 g za mbegu kavu kwa chumba kimoja cha fremu = gramu 45 za mbegu zilizolowa)



Mbegu safi na Bora



Mbegu iliyomea





Kusia Mbegu

Funika mbegu kwa kunyunyiza udongo mkavu kidogo juu ya mbegu



Mwagilia kwa kunyunyizia maji





Ondoa fremu taratibu ili kuitumia sehemu nyingine hadi eneo la kitalu linalohitajika likamilike.

**Kumwagilia kwa kutumia keni**



- Mwagilia kwa keni kwa siku tano za mwanzo (asubuhi na jioni)
- Ingiza maji kwenye mifereji ya pembeni kwa kitalu kilichonyanyuliwa kutoka siku ya 6 mpaka ya 14
- Kausha maji siku 2 kabla ya kuondoa mikeka ya miche kwa ajili ya kupandikiza



Miche michanga (umri wa siku 14-15 )

- Urefu wa miche = (sm 16-18)
- Urefu wa mizizi – sm 7-9
- Majani = 4-5
- Urefu wa majani = sm 10-12
- Miche yenye afya
- Rahisi kusafirisha na
- Rahisi kung'oa miche



Kusafirisha Miche



NIBIO MSSRF

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI)
Makao Makuu Makutupora,
Barabara ya Arusha,
S.L.P 1571, DODOMA
Baruapepe: info@tari.go.tz & dg@tari.go.tz
www.tari.go.tz